

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

UZINDUZI WA UZALISHAJI, USAFISHAJI NA USAFIRISHAJI GESI ASILIA KUPITIA MIUNDOMBINU MIPYA YA TAIFA KUFANYIKA TAREHE 29 JULAI 2015

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ilianza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia Juni, 2013. Miundombinu hii inajumuisha ujenzi wa mitambo miwili ya madimba na Songosongo ya kusafisha gesi asilia yenye uwezo wa kusafisha kiasi cha futi za ujazo milioni 350 kwa siku (350mmscfd) pamoja na bomba la kusafirisha gesi lenye urefu wa kilometa 542 kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam lenye uwezo wa kusafirisha futi za ujazo milioni 784 kwa siku (784mmscfd). Kwa kutumia mkandamizo bomba hili lina uwezo wa kusafirisha hadi futi za ujazo milioni 1002 kwa siku (1002 mmscfd)

TPDC inayofuraha kuufahamisha umma kuwa tarehe 29 Julai 2015, mitambo ya kusafisha gesi asilia pamoja na bomba la kusafirisha gesi asilia vitakua tayari kuanza majaribio ambayo yatachukua takribani siku arobaini (40) mpaka sitini (60). Kuanzia mwezi Septemba 2015, uzalishaji wa awali wa futi za ujazo milioni 80 kwa siku (80 mmscfd) kutoka katika visima vya kitalu cha Mnazi Bay kilichopo Mtwara utaanza. Baadae uzalishaji utaongezeka hadi kufikia futi za ujazo milioni 130 kwa siku (130mmscfd). Uzalishaji utaenda ukiongezeka kutoka katika visima vya Songo Songo ambapo inatarajiwa kutoa kiasi cha futi za ujazo milioni 120 kwa siku (120 mmscfd). Uzalishaji kutoka Songo Songo utarajiwa kuanza mwezi Oktoba 2015.

Ukamilishaji wa mradi huu ni moja ya hatua za makusudi za Serikali katika kuhakikisha uzalishaji wa umeme wa uhakika umekuwepo kwa kuongeza njia mbadala za kuzalisha nishati hiyo na pia kukuza matumizi mengine ya gesi asilia kama vile viwandani, majumbani na kwenye vyombo vya usafiri. Lengo kubwa likiwa ni kukuza uchumi wa nchi na kuondoa umasikini.

Taarifa imetolewa na:

**Mkurugenzi Mtendaji,
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania,
P.O.Box 2774,
Dar-es-Salaam.
Tanzania.**